**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS: TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO**

SHULE YA SEKONDARI MLONGWEMA,
S. L. P. 173,
LUSHOTO.
01/06/2023

Kumb.Na:**MSS/JI/ADV/V.1/2022/1**

**-------------------------------------------,**

**-------------------------------------------,**

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2023/2024 KATIKA SHULE YA SEKONDARI MLONGWEMA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO MKOA WA TANGA**

**SEHEMU A: UTANGULIZI**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule ya sekondari Mlongwema kwa mwaka 2023/2024 tahasusi ya
2. HGL/HKL
3. Shule ya sekondari Mlongwema ipo Mlola umbali wa kilometa 46, kaskazini mwa mji wa Lushoto. Ufikapo Lushoto mjini utapanda magari yanayoelekea Mlola kwa nauli ya shilingi elfu saba (7,000/=) tu.Ukifika Mlola panda pikipiki kwa shilingi elfu moja (1,000/=) tu hadi kufika shuleni.
4. Shule ya sekondari Mlongwema ni shule ya bweni kwa wasichana tu kwa kidato cha tano na sita na ya kutwa mchanganyiko kwa kidato cha kwanza hadi cha nne.
5. Ukiwa Mlongwema Sekondari, utalazimika kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu za Shule (kamilisha kiambatanisho B na C).
6. Utaripoti shuleni siku na tarehe **13/08/2023** na mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023.
7. Fika na nakala ya cheti cha kuzaliwa na nakala ya ***Result slip siku ya Kuripoti.***
   Kama huna cheti cha kuzaliwa, nenda Mahakamani ili **Uape upewe *Affidavit***, kuwa wewe ni raia waTanzania.

**SEHEMU B: SARE ZA SHULE NA MAHITAJI MENGINE**

***NB: KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA MKUU WA SHULE***

| NA. | SARE/MAHITAJI | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1 | Mashati 2 meupe ya Mikono Mifupi, Tetroni Lisiwe linalobana au linaloonesha ndani) | Anunue duka lolote |
| 2 | Sketi 2 ndefu hadi kwenye kiwiko mshono wa malinda (Dark Blue) | Unaweza kuzipata jirani kwa shuleni shuleni |
| 3 | Masweta 2 ya rangi ya kijani iliyo kolea (darkgreen) ya V (yasiwe ya vifungo) | Yanapatikana jirani na shuleni |
| 4 | Sweta au jacket zito jeusi 01 lisilo na kofia, picha Wala maandishi yoyote | Anunue duka lolote |
| 5 | Viatu vyeusi vya ngozi jozi 2 vya kufunga na kamba (visiwe vyenye visigino virefu), na soksi ndefu nyeupe jozi nne | Anunue duka lolote |
| 6 | Skafu moja ya rangi ya bluu iliyokolea (dark blue) | Inapatikana jirani na shuleni |
| 7 | Shuka 2 za rangi ya pink, Blanketi moja, foronya mbili na Chandarua moja ya rangi nyeupe. | Anunue duka lolote |
| 8 | Magauni mawili ya rangi ya kijivu (Grey) (shamba dress) yawe ya Kitambaa kizito kisichoonyesha nguo za ndani na hijab 2 nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama. (ya darasani) na kijivu mbili (kushindia). | Yanapatikana jirani na shuleni<br><br>Zinapatikanajirani na shuleni |
| 9 | Godoro imara la ukubwa wafuti mbili na nusu kwa sita ($2^1/_2$x6). (Godoro Dodoma au Comfy) | Anunue duka lolote |
| 10 | Picha 4 za passport size na file 2 (spring files) | Apige popote, anunue popote |
| 11 | Picha nne passport size za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu | Apige popote |
| 12 | T–shirt 1 ya rangi ya bluu ya mawingu isiyo na Maandishi yoyote (kushindia) | Inapatikana jirani na shuleni |
| | T–shirt 1 ya damu ya mzee yenye nembo ya shule ya sekondari Mlongwema (kwa ajili ya darasani kwa siku maalumu) | Inapatikana jirani na shuleni |
| 13 | Track suit ya rangi ya bluu ya mawingu (light skyblue) na raba nyeupe kwa ajili ya michezo | Inapatikana jirani na shuleni |
| 14 | Sanduku imara la bati (tranker) kwa ajili ya Kuhifadhia vifaa vyake | Anunue duka lolote |
| 15 | Vifaa vya chakula ikiwa ni pamoja na Kijiko, sahani, kikombe na bakuli | Anunue duka lolote ila visiwe Vya plastiki |

| | | |
|---|---|---|
| 16 | Ndoo ndogo moja lita 10 na kubwa moja lita 20 (kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa. Zote ziwe zenye mfuniko. | Anunue duka lolote |

| | | |
|---|---|---|
| 17 | Vifaa vya usafi vikiwa ni pamoja na jembe 1 lenye mpini, mopper 1(ndoo na mopper), mifagio (hardbroom) 2, Fagio la chelewa 1 na squeezer 1 . | Anunue duka lolote |
| 18 | Rimu mbili (A4) kwa kidato cha tano na rimu mbili (A4) kwa kidato cha sita. (atatoa rimu mbili kwa ajili ya kidato cha tano tu) | Anunue popote |
| 19 | Aje na bima ya afya (NHIF/CHF) au Pesa taslimu kwa ajili ya kukatiwa bima ya CHF akiwa shuleni. (Tsh. 5000 kwa ajili ya CHF na 5000 kwa ajili ya huduma za dharura. Lakini pia aje na Tsh. 1000 kwa ajili ya kulipia control number ya bima ya kaya (CHF) | Kama ana bima aidha NHIF au CHF aje na Tsh 5000 tu kwa ajili ya huduma za dharura |

BEI YA VIFAA VINAVYOPATIKANA SHULENI

1. Sketi 2 kila moja Tsh. 27,000/= jumla Tsh. 54,000/=
2. Sweta 2 kila moja Tsh. 15,000/= jumla Tsh. 30,000/=
3. Shamba dress 2 kila moja Tsh. 27,000/= jumla 54,000/=
4. Track suit 2 kila moja 27,000/= jumla Tsh. 54.000/=
5. Skafu 1 tsh. 3000
6. T-shirt ya darasani Tsh. 15,000/=
7. T-shirt ya kushindia Tsh. 15,000/=
8. Hijab 2 ya darasani (nyeupe) na ya kushindia (kijivu) @ Tsh 16,000/= jumla 32,000/=

**SEHEMU C: VIFAA VYA DARASANI.**

1) Afike na daftari (counter books) saba, kalamu, mkebe (Mathematical Set) na scientific calculator kwa watakaosoma somo la Jiografia.
2) Dictionary 1 ya kingereza kwa kingereza, kamusi ya Kiswahili 1 na ya Kiswahili kwa kingereza 1 kwa matumizi binafsi na kwa masomo ya tafsiri na ukalimani kwa somo la kingereza na kiswahili.
3) Mwanafunzi anayesoma KISWAHILI NA ENGLISH LANGUAGE anapaswa kuja na vitabu vya fasihi vinavyosomwa darasani.

**VITABU VYA FASIHI KATIKA SOMO LA KISWAHILI**

**USHAIRI**

1. Kimbunga...................................................... Haji Gora
2. Mapenzi Bora............................................... Shaban Robert
3. Chungu Tamu...................................................Theobald A. Mvungi
4. Fungate Ya Uhuru............................................ Shafii Adam Shafii

**RIWAYA**

1. Usiku Utakapokwisha ......................................Mbunda Msokile
2. Kufikirika............................................................ Shaban Robert
3. Mfadhili.................................................................Hussein Tuwa
4. Vuta N’kuvute.................................................. Shafii Adam Shafii

**TAMTHILIYA**

1. Nguzo Mama.............................................. Penina Mhando
2. Kwenye Ukingo Wa Thim ............................Ebrahim Hussein
3. Morani......................................................... Emmanuel Mbogo
4. Kivuli Kinaishi........................................... Saidi Mohamed

**LITERATURE BOOKS**

**NOVEL AND SHORT STORIES**

- The Beautiful Once Are Not Yet Born .............Ayi Kwei Armah
- A Man Of The People ........................................Chinua Achebe
- Divine Providence............................................. Sevirin N. Ndunguru
- His Excellency The Head Of State .....................Danny Safo
- Vanishing Shadows............................................. Namige Kayondo
- The Rape Of The Pearl.........................................Magala Nyago

**PLAYS**

- Betrayal in the City .............................................Francis Imbuga
- I Will Marry When I want ..................................Ngungi wa Thiong'o and Ngungi wa Mirii
- An Enemy Of the People ..................................Henrik Ibsen

**POETRY**

- Selected Poems .....................................Tanzania Institute of Education (TIE)
- The Wonderful Surgeon and Other Poems ..................Charles Mloka

Angalizo . **Anunue vitabu vyake kwa ajili ya kujisomea kwani shule haina vitabu vya kutosha.**

**SEHEMU D: MICHANGO YA SHULE**

**(LIPA KWENYE AKAUNTI YA NMB NAMBA 41603500042 YENYE JINA LA MLONGWEMA SECONDARY SCHOOL FUND)**


| Na | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1 | Kitambulisho cha mwanafunzi | 5,000 |
| 2 | Tahadhari(hairudishwi) | 5,000 |
| 3 | Nembo ya shule | 5,000 |
| 4 | Michango ya uendeshaji wa shule | 65,000 |
| | **Jumla** | **80,000** |

**MUHIMU:**

1. Michango yote inalipwa benki (hatupokei pesa taslimu)
2. Mwanafunzi aje na risiti ya malipo ya benki (bank pay in slip)
3. Mwanafunzi atapokelewa tu iwapo amekamilisha kulipa michango na kukabidhi vifaa vyote vilivyo agizwa.
4. Mwanafunzi anashauriwa kuwa awe na fedha za mfukoni (pocket money) kwa ajili ya matumizi binafsi.
5. Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni akiwa na bima ya afya au fedha ya kutosha kwa ajili ya matibabu pale atakapougua. Shule inatoa huduma ya kwanza tu (tunashauri zaidi mzazi mkatie mwanao bima ya afya ili kuondoa usumbufu).



**MWITANGO L. MSWAKI**
**MKUU WA SHULE**



**SIMU:**
**MKUU WA SHULE: 0718 618 330**
**MAKAMU MKUU WA SHULE: 0764 599 993**

**KIAMBATANISHO A:**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULEYASEKONDARIMLONGWEMA

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yafuatayo yatasababisha mwanafunzi kufukuzwa shule mara moja:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
**vi.** Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule; **Shule hairuhusu kusuka nywele kwa namna yoyote ile.**
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**ANGALIZO**

Ni jukumu la mwanafunzi kufuata sheria, taratibu na kanuni zilizo wekwa pamoja na nyingine atakazoelekezwa ili kuepuka adhabu na kufukuzwa shule.

Walimu shuleni ni waelekezaji, walezi, waelimishaji na washauri wa wanafunzi.

Mwanafunzi akiwasikiliza atafika kule anakotarajia/anakopanga kufika. Mtu hawezi kudai kuwa anaelimika wakati hana tabia inayokubalika katika jamii yake. Licha ya elimu yake mtu huyu atakuwa ‘**msungo’.**

**KIAMBATANISHO B**

*The united Republic of Tanzania*

**President's Office: Regional Administration and Local Government**

Mlongwema Secondary School,
P. O. BOX 173,
LUSHOTO
01/06/2023
,

To the Medical Officer,
……………………………………,
……………………………………..
………………………………………..
………………………………………

**<u>Ref: A STUDENT'S MEDICAL EXAMINATIONS FORM</u>**

Please, examine the student……………………………………………………… in respect of these areas and
Any other area (s) deemed fit Please. Delete whichever not applies.
Does the Student have problems in connection with………………………………………………………?

a) Sight Yes/No. If yes, state…………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..

b) Hearing. Yes/No. If yes, state………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………

c) T.B or any other Chronic Diseases. Yes/No. If yes, state…
……………………………………………………………………………………………………..

a) Blood Pressure. Yes/No. If yes, state ……………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………….

b) Diabetes. Yes/No. if yes state ………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………………..

c) Any Physical Impairment (s). Yes/No. If yes, state ……………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………………..

d) Do you therefore recommend this student to pursue studies at this school?
……………………………………………………………………………………………………….

Name……………………………………….. Signature……………….. Date: …………………

Official Title……………………………….. Official Stamp……………………………………………

**KIAMBATANISHO C**

JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO SHULE YA SEKONDARI MLONGWEMA

**I: TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. JINA KAMILI: ……………………………………………
2. TAREHE YA KUZALIWA: …………………………..
3. URAIA: ………………………………
4. DINI: ………………………………
5. SHULE ULIYOSOMA:
   JINA LA SHULE: ……………………………………..
   MWAKA WA KUANZA: …………….. MWAKA WA KUMALIZA: ……….
   SAHIHI YA MWANAFUNZI: …………………….. TAREHE:…………………..

**II: MAELEZO YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI KUKIRI NA KUKUBALIANA NA SHERIA KANUNI NA KULIPA ADA, MICHANGO MINGINE NA MAELEKEZO MENGINE YA SHULE**

1. JINA LA BABA MZAZI/MLEZI: …………………………………………………….
   MKOA: …………………. WILAYA: ………………….KATA:………………
   KIJIJI/MTAA: ……………………. S.L. P ………………….. SIMU…………………
   KAZI YA MZAZI/MLEZI: ……………………………………………….
2. JINA LA MAMA MZAZI/MLEZI: ……………………………………………….
   MKOA: …………………. WILAYA: ………………….KATA:………………
   KIJIJI/MTAA: ……………………. S.L. P………………….. SIMU…………………
   KAZI YA MZAZI/MLEZI: ……………………………………………….

   **MAELEZO YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

   Mimi… ……………………………………….. ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……………………………………………nimesoma na kuelewa maelezo yote yaliyotolewa kuhusu sheria, kanuni, ada na michango ya shule. Ninakubali mwanangu ajiunge na shule ya Sekondari Mlongwema na ninaahidi kulipa ada na michango hiyo pamoja na kutekeleza maelekezo mengine yatakayotolewa na shule ikiwa ni pamoja na kutompatia mwanafunzi simu na endapo atabainika kuwa na simu anastahili kufukuzwa shule kwa mujibu wa kanuni na sheria za shule.

   Jina……………………………………….. Saini……………………………
   Tarehe……………………………….

**KIAMBATANISHO D**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI MLONGWEMA
PICHA NA NAMBA ZA SIMU ZA WAZAZI/WALEZI NA NDUGU WATAKAOWASILANA NA MWANAFUNZI AU KUFIKA KUMUONA AWAPO SHULENI.

1

JINA…………………………………
UHUSIANO NA MWANAFUN ZI………………
NAMABA YA SIMU……………… ……

2

JINA……………………………………………..…
UHUSIANO NA MWANAFUNZI ………………
NAMBA YA SIMU…………………….…………

3

JINA………………….……………
UHUSIANO NA MWANAFUNZI…………….
NAMABA YA SIMU……………………….…

4

JINA…………………..………………
UHUSIANO NA MWANAFUNZI…………
NAMBA YA SIMU………………………

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0718 618 330**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0764 599 993**
- **Mwandamizi Taaluma: 0755 358 212**
- **Mwandamizi Malezi (Matron): 0652 555 225**